**MKATABA WA RAMSAR WA USIMAMIZI WA MAENEO YA ARDHI OEVU (RAMSAR. CONVETION ON WETLANDS).**

## 1. Utangulizi

Mkataba wa Ramsar kuhusu ardhi oevu ni mkataba wa kimataifa wa mazingira unaolenga kulinda na kuhakikisha matumizi endelevu ya ardhi oevu duniani. Mkataba huu unatambua umuhimu mkubwa wa ardhi oevu katika kuhifadhi bioanuai, kusaidia shughuli za kiuchumi, kudhibiti majanga ya asili kama mafuriko, na kuchangia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Ulisainiwa mwaka 1971 huko Ramsar, Iran, na kuanza kutumika rasmi mwaka 1975. Mkataba wa Ramsar una jumla ya nchi wanachama 172 duniani. Tanzania ilijiunga rasmi na Mkataba huu tarehe 13 Agosti 2000.

## 2. Ushiriki wa mikutano kwa nchi wanachama

Nchi wanachama wa Mkataba wa Ramsar hushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa kwa lengo la kujadili utekelezaji wa Mkataba, kubadilishana uzoefu, na kuweka mikakati ya pamoja ya kuhifadhi na kutumia kwa ufasaha ardhi oevu. Mikutano ya nchi wanachama (Conference of the Parties – COP), hufanyika kila baada ya miaka mitatu.

## 3. MALENGO YA MKATABA

Malengo makuu ya Mkataba wa Ramsar ni:

- Kuhifadhi ardhi oevu na kuhakikisha zinatumika kwa njia endelevu;
- Kulinda bioanuai inayopatikana katika ardhi oevu;
- Kudumisha hali ya kiikolojia ya ardhi oevu;
- Kukuza ushirikiano wa kimataifa katika usimamizi wa rasilimali za maji na ardhi oevu;
- Kusaidia maendeleo endelevu yanayozingatia uhifadhi wa mazingira.

## 4. MAJUKUMU YA NCHI WANACHAMA

i. Kutambua na kuteua maeneo ya ardhi oevu yenye umuhimu wa kimataifa (Ramsar Sites);
ii. Kusimamia na kulinda ardhi oevu kwa kutumia sera na sheria za kitaifa;
iii. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Mkataba mara kwa mara;
iv. Kukuza uelewa kwa umma kuhusu umuhimu wa ardhi oevu;
v. Kushirikiana na nchi nyingine katika usimamizi wa rasilimali za pamoja;

## 5. FURSA ZITOKANAZO NA MKATABA

- ❖ Uanachama katika Mkataba huu hutoa fursa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:
- ❖ Upatikanaji wa msaada wa kitaalamu na miongozo ya kimataifa;
- ❖ Fursa za ufadhili na uwekezaji katika miradi ya mazingira;
- ❖ Kuimarisha uwezo wa kitaifa katika usimamizi wa ardhi oevu;
- ❖ Kukuza utalii wa ikolojia na kipato kwa jamii;
- ❖ Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa;
- ❖ Kuchangia juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## 6. MAFANIKIO YA MKATABA

- kutambuliwa kwa maeneo muhimu ya ardhi oevu kama Ramsar Sites, ambayo ni:
    - Muyovozi – Mto Malagarasi (Kigoma);
    - Bonde la Ziwa Natron (Manyara);
    - Bonde la Mto Kilombero (Morogoro);
    - Ukanda wa Pwani wa Rufiji–Mafia–Kilwa.
- Kuimarika kwa sera na mikakati ya usimamizi wa ardhi oevu katika nchi wanachama;
- Kuongezeka kwa uelewa wa umuhimu wa ardhi oevu;
- Kuanzishwa kwa miradi ya uhifadhi na matumizi endelevu ya ardhi oevu;
- Kuimarika kwa ushirikiano wa kimataifa katika uhifadhi wa bioanuai.

## 7. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI

Pamoja na mafanikio, utekelezaji wa Mkataba unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

- Uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa ardhi oevu;
- Shughuli za kibinadamu zisizo endelevu kama kilimo holela na ujenzi;
- Uvamizi wa ardhi oevu;
- Ukosefu wa rasilimali za kutosha (fedha na wataalamu);
- Uratibu hafifu kati ya taasisi mbalimbali;
- Athari za mabadiliko ya tabianchi;
- Uwepo wa spishi vamizi zinazoathiri mifumo ya ikolojia.